

Utetezi

MAMBO AMBAYO KURANI HUFUNDISHA KUHUSU BIBLIA

Mwandishi Ndugu Andy

Sehemu mbili kuu za Biblia, yaani Agano la Kale na Agano Jipya, huitwa "*Taurat*" [Torati] na "*Injil*" [Injili], maana yake Sheria na Habari Njema, katika Kurani. Hutofautisha sehemu hizo na kutambua *Taurat* kama Maandiko Matakatiifu ya Wayahudi na *Injil* kama Maandiko Matakatiifu ya Wakristo. Kuhusu Wayahudi, Muhammad alielezwa katika Sura 5:43: "Na watakuwekaje wewe kuwa hakimu, nao wanayo Taurati yenye hukumu za Mwenyezi Mungu?" (S. 5:43)

Tamko hili linaonyesha wazi kwamba Wayahudi walikuwa na Torati wakati wa Muhammad na kwamba ilikuwa na mafunuo ya Mungu. Hakuna hata dokezo katika Kurani kwamba Biblia ilibadilishwa kwa njia yoyote ile. Mara fulani Kurani inawashtaki Wayahudi kwamba walificha ukweli (3:71), kugeuza maana ya Torati kwa ndimi zao (3:78) na kutunga maandiko yao wenyewe wakidai kwamba ni sehemu ya Torati (2:79). Lakini hakuna mahali popote ambapo Kurani huwashtaki kwamba walibadilisha Torati!

Kurani husema: "Hakika tuliteremsha Taurati yenye uwongozi na nuru" (S. 5:44)

"Na bila shaka tulimpa Musa Kitabu - basi usiwe na shaka na kukutana na Mwenyezi Mungu - na tukakifanya uwongofu kwa wana wa Israili, (Mayahudi)." (S. 32:23)

(note - 23 not 22 as printed)

Inaonekana kwa jinsi Kurani inavyoeleza kwamba *Taurat* kilikuwa kitabu kilichoteremshwa kwa Musa (*Nazil*) lakini katika historia hakuna habari yoyote ya mafunuo kama hayo. Wala Kurani haidokezi popote kwamba *Taurat* ni kitabu kingine kuliko kile ambacho Wayahudi wenyewe wanakikubali kuwa ndicho Torati, kwa hiyo tuna uthibitisho wazi kutoka katika Kurani yenyewe kwamba Agano la Kale ni Neno la Mungu la kweli lisilobadilishwa.

Wakristo hutambua Agano Jipya kwa jumla na mafunzo yake yote kuwa ndiyo Injili (Marko 1:1, Warumi 1:1). Pia, Kurani hukiri kwamba Wakristo walikuwa na *Injil* wakati wa Muhammad, na kushuhudia kwamba Agano Jipya ndilo Neno la Mungu:

"Na Tukawafuatishia (Mitume hiyo) Isa bin Maryamu kuyahakikisha yaliyokuwa kabla yake katika Taurati, na tukampa Injili iliyomo ndani yake uwongozi na nuru na isadikishayo yaliyokuwa kabla yake katika Taurati, na uwongozi na mauidha kwa wamchao (wanaomwogopa).

Watu wa Injili wahukumu kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu ndani yake. Na wasiohukumu kwa (kufuata) yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu basi hao ndio maasi."

(S. 5:46,47)

Note: Both verses not only 47, and I have quoted the whole of 47 not half of it.

Mstari wa kimsingi katika Kurani ambao hutilia mkazo kuaminika kwa Biblia ni huu:

"Sema: 'Enyi watu wa Kitabu! Hamko juu ya cho chote (katika dini yenu) mpaka msimamisha Taurati na Injili na haya yaliyoteremshwa kwenu kutoka kwa Mola wenu" (S.5.68)

Note: the Swahili Koran immediately adds after "Mola wenu: (Nayo ni Qurani) i.e. "Which is the Koran" thus effectively cancelling the message of the sentence itself. This makes it a doubtful text to use in talking to a Muslim.

Zaidi ya hayo, Kurani huwa na mistari fulani iliyokaririwa kutoka katika Biblia, pamoja na kukiri imetoka wapi. (S.5:45 = Kutoka 21:23-25: "Na humo (katika Taurati) tuliwaandikia ya kwamba mtu (huuawa) kwa mtu, na jicho hutofolewa) kwa jicho, na pua (hukatwa kwa pua, na sikio (humeguliwa) kwa sikio, na jino (hung'olewa) kwa jino..." S.7:40 = Mathayo 19:24: "...wala hawataingia Peponi mpaka aingie ngamia katika tundu ya sindano...".)

Tukitafakari mistari ile yote katika Kurani inayoeleza habari za Torati na Injili, tunaweza kufikia maamuzi yafuatayo:

- 1) Wakati wa Muhammad nakala za Agano la Kale na Agano Jipya, pamoja na Torati, Zaburi, vitabu vya Manabii na Injili, zilikuwepo kati ya Wayahudi na Wakristo.
- 2) Kurani yenyewe inatamka wazi kwamba vitabu hivyo vilitoka kwa Mungu.
- 3) Kurani, ambayo hujidai kuwa imetokana na upuzio wa kiroho wa hali ya juu kabisa, hutambua Biblia kwamba imetokana na upuzio huo huo.
- 4) Kurani huita Biblia majina muhimu sana: Kitabu cha Mungu, Neno la Mungu, Nuru, Uwongozi, Rehema.
- 5) Kurani hufundisha kwamba Muhammad aliagizwa na Mungu akubali ushuhuda wa Biblia na kuwaambia Wayahudi na Wakristo waifuate kama Uongozi wao.
- 6) Waislamu wanaagizwa katika Kurani wakiri kwamba wanaamini Biblia kama vile wanavyoamini Kurani.

7) Adhabu za kutisha kabisa katika ulimwengu ujao zinatajwa kwa ajili ya watu wanaokataa ama Biblia ama Kurani (S. 40:69-72)

In the Swahili version the matching verses are 69-72 not 72-73.